

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAISI-TAMISEMI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI



**Namba za simu:**

Mkuu wa Shule: **0756510222**

Makamu Mkuu wa Shule: **0757635500**

Matron/patron: **0752227218**

Shule ya Sekondari Milundikwa,  
S.L.P 634,

**Sumbawanga,**

Tarehe.....

Mzazi/Mlezi wa **Mwanafunzi**.....

.....

S.L.P.....

.....

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA  
SEKONDARI MILUNDIKWA HALMASHAURI YA  
NKASI MKOA WA RUKWA MWAKA 2017**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2018 tahasusi ya..... Shule ya sekondari Milundikwa ipo umbali wa kilometa 50 Kaskazini Magharibi mwa mji wa Sumbawanga. Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi kwa nauli ya **sh.4000/=** kwa wale wanaotokea barabara ya Mpanda Sumbawanga washukie kijiji cha Kasu ndipo shule ilipo.

Muhula wa masomo unaanza tarehe.....  
hivyo mwanafunzi anatakiwa kulipoti shuleni tarehe.....  
Mwisho wa kuripoti ni tarehe.....

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare ya shule

- a) Sare ya shule hii ni: sketi ya dark blue na kaki yenye linda box moja kubwa mbele na nyuma na iwe ndefu mpaka chini
- b) Rangi ya hijabu iwe nyeupe.(kwa wanafunzi wa Dini ya Kiislamu)
- c) Sare ya michezo kwa shule hii ni tracsuit ya blue
- d) Viatu vya shule ni nyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
- e) Soksi jozi mbili nyeupe.
- f) Sweta rangi ya blue.
- g) Nguo za kushindia(shamba dress) rangi ya pinki yenye drafti ndogo
- h) Tai ya kaki na dark blue.

### 2.2. Ada na Michango ya Shule

- a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi **70,000/=** kwa mwanafunzi wa bwani. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi **35,000/=** kwa mwanafunzi wa bwani kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja.
- b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-
  - i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
  - ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
  - iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
  - iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa walipishi, walinzi na vibarua wengine
  - v. Shilingi 2,000/= Nembo ya shule
  - vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza, Tshs. 5,000/= na Bima ya Afya Tshs. 5,000/= (wanafunzi washauriwe kujiunga na mfuko wa Bima ya Afya CHF kikaya)
  - vii. Shilingi 20,000/= Mitihani ya kujipima(mock)
  - viii. Fedha ya tahadhari Tshs. 5,000/= (haitarejeshwa)
  - ix. Ada ya mtihani wa Taifa ni shilling 50,000/=

**NB:** Fedha hizo zote zilipwe kwenye Akaunti ya shule **Na: 62010001128 Milundikwa Secondary school Development Account** katika benki ya **NMB** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip)

- C. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuketa shule ni:-
  - i. Ream ya karatasi 1(kwa mwaka)2
  - ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
  - iii. Godoro la t 2<sup>1/2</sup>
  - iv. Mashuka pair 2 light blue, Blanketi 1, Foronya 1, Chandarua 1

- v. Vyombo vya chakula (sahani,Bakuli,Kijiko na kikombe)
- vi. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
- vii. Kwanja 1, jembe 1, mifagio ya ndani na nje.

**3. MAKOSA YATAKAYO MSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:**

- i. Wizi
- ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
- iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
- iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu ,walezi na jamii kwa ujumla
- v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpinga mwalimu au mtu yeyote Yule
- vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
- vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
- viii. Uvutaji wa sigara
- ix. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuo au kuolewa
- x. Kupata ujauzito au kutoa mimba
- xi. Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yanayovunja sheria za nchi.
- xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
- xiii. Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
- xiv. Kudara bendela ya Taifa
- xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n,k
- xvi. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

4. Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilii

**KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya MKuu wa Shule .....**

**Jina la Mkuu wa Shule .....**

**Mhuri wa MKuu wa Shule .....**